# JARIDA LA RS RUVUMA

TOLEO LA APRILI 2025



## Mwenge wa Uhuru kuanza mbio zake Ruvuma Mei 9



## KARIBU MKOA WA RUVUMA

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

## JARIDA LA RS RUVUMA TOLEO LA APRILI 2025

Jarida limehaririwa na **Albano Midelo** wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma



## TAHARIRI

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.

Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wa ngazi ya Wilaya,Mkoa na kitaifa wanavyofanya ziara za kuzungumza na wananchi,kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma

## MBIO ZA MWENGE WA UHURU KUANZA RUVUMA MEI TISA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amesema kuwa mbio za mwenge mkoani Ruvuma zitaanza tarehe 9 Mei, 2025 ambapo mwenge huo utapokelewa katika Kijiji cha Igawisenga, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, ukitokea Mkoani Njombe.

Akizungumza na waandishi wa habari Ofisini kwake, Kanali Ahmed amesema ni muhimu kwa wananchi wa mkoa wa Ruvuma kufahamu kuwa mwenge huo utakimbizwa katika halmashauri zote nane za mkoa wa Ruvuma.

Ametaja ratiba ya mbio hizo katika mkoa wa Ruvuma ambapo Mei 9, 2025 ni Madaba DC, Mei 10, 2025 Songea DC, Mei 11, 2025 Mbinga DC, Mei 12, 2025 Nyasa DC, Mei 13, 2025 Mbinga TC, Mei 14, 2025 Songea MC, Mei 15, 2025 Namtumbo DC, Mei 16, 2025 Tunduru DC na tarehe 17 Mei 2025 mwenge huo utakabidhiwa mkoa wa Mtwara.

Kanali Ahmed ameeleza kuwa pamoja na mambo mengine, kutakuwa na midahalo mbalimbali inayogusa maendeleo na maisha ya wananchi. Amehimiza wananchi wa Ruvuma, wadau wa maendeleo, sekta za umma na binafsi kujitokeza kushiriki mbio hizo na kutumia fursa hiyo kutangaza na kuonyesha shughuli zao kupitia sehemu za mikesha ambazo zitakuwa zimeandaliwa.

Mbio hizo kwa mwaka huu zinaongozwa na kauli mbiu inayohusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambayo inasema "Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu," kauli mbiu hiyo inaambatana na ujumbe wa kudumu wa mapambano dhidi ya Malaria unaosema "Zero Malaria inaanza na mimi, wewe na sisi wote."

Kauli mbiu zingine ni "Kataa dawa za kulevya, timiza malengo yako," "Kuzuia rushwa ni jukumu langu na lako, tutimize wajibu wetu," na ujumbe unaohusu lishe unaosema "Afya ni mtaji wako, zingatia unachokula."



# DC SONGEA AONGOZA MAADHIMISHO MIAKA 61 YA MUUNGANO



Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, amewaongoza wananchi wa Wilaya ya Songea kuadhimisha miaka 61 ya Muungano wa Tanzania, ambapo tarehe 26 Aprili 1964 nchi ya Tanganyika na Zanzibar ziliungana.

Maadhimisho hayo ambayo yalitanguliwa na shughuli mbalimbali kama upandaji wa miti na usafi wa mazingira katika Wilaya ya Songea, yalianza kwa maandamano ya amani na kuhitimishwa kwa hafla fupi katika viwanja ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wa Songea iliyopo manispaa ya Songea.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mhe. Ndile, amesema wananchi wanapaswa kujua Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni jitihada za watu na viongozi wa Tanganyika na Zanzibar zilizofanyika ili kulifanya Taifa liwe moja, lenye watu wanaoheshimiana, wanaoelewana na kuthaminiana utu.

Ameongeza kuwa kama Taifa linatakiwa kujivunia umoja na mshikamano uliopo baina ya watu wote nchini bila kujali desturi na maeneo wanayotokea kwa kuwa ndio msingi imara wa amani katika Taifa.

Ametoa wito kwa watumishi wa umma na wananchi wote kuwa watiifu na waaminifu kwa Taifa na kuepuka kutoa kauli ambazo zinaweza kusababisha uvunjifu wa amani ili kuhakikisha Taifa linaepuka machafuko yayiso na msingi.

Akitoa historia ya Muungano wa Tanzania, Mwenyekiti wa Wazee Wilaya ya Songea, Sofia Namananda, amesema waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Abeid Aman Karume, walikuwa na maono ya mbali katika kuhakikisha nchi inakuwa na mshikamano na umoja wa kujenga Taifa Moja la Tanzania.

Ameeleza kuwa hivi sasa Taifa linajivunia matunda ya nguvu walizotumia waasisi hao, kwa kuwa walifanya kazi kubwa mpaka hivi sasa wananchi wanaishi kwa amani na utulivu, hivyo wanaliombea Taifa liendelee kuwa na amani na utulivu.

Kwa upande wake Mkazi wa Wilaya ya Songea, Mohamed Kwizombe, amesema maadhimisho ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania kama mwananchi anajivunia amani na utulivu uliopo katika Taifa hivyo amani idumishwe hadi kufikia vizazi vijavyo.

Maadhimisho hayo ya miaka 61 ya Muungano wa Tanzania, ambao ulifanyika Arili 26, 1964 na kuasisiwa na Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Aman Karume, kwa mwaka huu wa 2025 yameongozwa na kauli mbiu inayosema " Muungano Wetu ni Dhamana, Heshima na Tunu ya Taifa , Shiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka

2025".

**MSITU WA MWAMBESI HAZINA YA ASILI INAYOTANGAZA UTUKUFU WA RUVUMA**



Msitu wa Hifadhi ya Taifa wa Mazingira Asilia Mwambesi, ulioko pembezoni mwa Mto Ruvuma wilayani Tunduru, umeibuka kuwa lulu ya kipekee ya kihistoria, kiasili na kiutalii inayolipa heshima kubwa Mkoa wa Ruvuma. Ukiwa na ukubwa wa zaidi ya hekta 112,000, msitu huu ulioanzishwa mwaka 1956 na kupandishwa hadhi

mwaka 2017/2018, umehifadhi viumbe adimu na mazingira hai ya kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Meneja wa TFS Wilaya ya Tunduru, Denis Mwangama, Mwambesi ni makazi salama kwa wanyama wakubwa kama tembo, simba, nyati na chui, lakini pia ni hifadhi pekee duniani kwa ndege wa ajabu aitwaye Pentiole, aliyehamia kutoka Madagaska. Ndege huyu hupatikana katika Maporomoko ya Sunda, ambapo huogelea kwenye maji akisaka samaki hai, kitendo cha kipekee kinachovutia wapenzi wa utalii wa kiikolojia.

Mbali na vivutio vya sasa, Mwambesi pia ni kumbukumbu hai ya historia ya vita ya Majimaji, ambapo mapango juu ya maporomoko ya Sunda yalitumika na wapiganaji kujificha. Mto Ruvuma ulikuwa chanzo muhimu cha maji na njia ya biashara ya kihistoria ya meno ya tembo na watumwa kati ya Msumbiji na Tanzania wakati wa utawala wa Wajerumani na Waarabu.

Deborah Mwakanosya wa TFS anabainisha kuwa Mwambesi ni msitu wa pili kwa ukubwa Tanzania na umejaa mimea ya nadra kama mipozipozi, pamoja na wanyama wa majini kama mamba na viboko. Watalii wana nafasi ya kuendesha mitumbwi Mto Ruvuma na kushuhudia mandhari ya kuvutia ya fukwe za asili na maisha ya porini yaliyo salama kwa uhifadhi endelevu.

Kabla ya kuwa hifadhi, eneo hili lilitumika kwa uwindaji wa kitalii kupitia kampuni ya Tandara Hunting Safaris. Hata hivyo, sasa Mwambesi umebadilika kuwa kituo cha uhifadhi wa kimataifa chenye dira ya kuhifadhi mazingira, kuendeleza utalii wa asili na kurithisha kizazi kijacho urithi wa asili na historia ya taifa.



***Maporomoko ya  Mto Ruvuma ya Nakatuta katika Pori la Akiba Liparamba Nyasa***

## MTO RUVUMA MOYO WA UTALII KUSINI



Ukitaka kushuhudia maajabu ya asili, historia ya ukombozi wa Afrika, na uzuri wa utalii wa kipekee unaovutia kwa macho na roho, basi safari yako lazima ipitie Mto Ruvuma ,mto mrefu kuliko yote Afrika Mashariki na kati.

Mto Ruvuma ni mto ambao haupokei sifa kwa ukubwa wake pekee, ukiwa na urefu wa zaidi ya kilomita 800 na upana wa hadi mita 720 .

Kama simulizi ya hadithi za kale, chanzo cha Mto Ruvuma kipo katika milima ya Matogoro, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Kisima kidogo tu kilicho meta 1500 kutoka usawa wa bahari. Lakini kutoka hapo, mfereji huo mdogo huanza safari ya kuandika historia katika wilaya zote tano za Mkoa wa Ruvuma: Songea, Mbinga, Nyasa, Namtumbo na Tunduru.

Mto Ruvuma si mto tu wa kupendezesha mandhari; ni moyo unaodunda kwa jamii na viumbe hai kusini

### *Fukwe, Visiwa na Wanyama Pori*

Kuelekea wilaya ya Namtumbo na Tunduru, Mto Ruvuma hubadilika kuwa mto wa ndoto kwa watalii.

Hifadhi ya mazingira asilia ya Mwambesi inatoa mandhari ya kipekee ,visiwa vidogo, fukwe nzuri, na safari za mitumbwi.

Hapa, tembo, simba, swala, mamba, na samaki wa aina mbalimbali hutawala kando mwa Mto Ruvuma wakivutia watalii kutoka ndani na nje ya nchi.

Katika Pori la Akiba la Liparamba wilayani Nyasa, maporomoko ya Nakatuta ni kivutio kingine. Wageni huja kuvua samaki, kupiga picha, na kupanda miamba ya asili iliyobeba historia ya miaka mingi.

***Historia Iliyogubikwa na Maajabu***

Mto Ruvuma haujaishia kwenye uzuri wa kiasili pekee; ni shahidi wa harakati za uhuru. Katika eneo la Mwambesi, maji haya yalitumika katika Vita ya Majimaji (1905–1907), na maporomoko ya Sunda yalitumika kama "darubini ya vita ya porini" ya Golira War iliyopiganwa Msumbiji.

Katika eneo hili, ndege mdogo zaidi duniani pantiole huogelea na kuwinda samaki hai, tukio adimu la kihistoria na kibaiolojia.

Safari ya Mto Ruvuma inaendelea katika daraja la Umoja, mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, wilayani Nanyumbu. Daraja hilo lenye urefu wa zaidi ya meta 700 linaunganisha mataifa mawili  na siyo kwa daraja pekee, bali kwa urithi wa pamoja wa historia, utalii na amani.

***Bahari ya Hindi: Hitimisho la Safari***

Mwisho wa safari ya Mto Ruvuma ni katika Bahari ya Hindi, eneo la Msimbati, Mtwara. Hapa, maji ya mto huingia katika Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma

Hakuna shaka Mto Ruvuma si tu kivutio, bali ni chemchemi ya uhai kwa Watanzania na majirani zao wa Msumbiji.



## WANANCHI NAMTUMBO WAPATA GARI LA WAGONJWA




Wananchi wa vijiji vya Magazini, Sasawala, Amani na Likusanguse wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma wameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwapatia gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Magazini, hatua ambayo wamesema itapunguza vifo vinavyotokana na ucheleweshwaji wa huduma za rufaa.

Kituo hicho kiko umbali wa zaidi ya kilomita 230 kutoka makao makuu ya wilaya hiyo ambapo ndipo ilipo hospitali ya Serikali ya Wilaya ya Namtumbo.

Wakizungumza kwenye hafla ya makabidhiano, wananchi walionesha furaha yao mbele ya Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, Mheshimiwa Vita Kawawa, ambaye ndiye aliyekabidhi gari hilo.

Chifu wa kabila la Wayao katika eneo la Magazini, Thabiti Shaibu Nnambi, alisema wamepoteza zaidi ya watu kumi kutokana na ukosefu wa gari la wagonjwa.

Alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mbunge Kawawa kwa juhudi za kuhakikisha huduma bora zinawafikia wananchi wa maeneo ya mbali kama Magazini.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dr.Aron Hyela, alieleza kuwa Kituo cha Afya cha Magazini ni miongoni mwa vituo 60 vya huduma

za afya wilayani humo na kimepokea zaidi ya Shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali

## HIFADHI YA NYERERE KUFUNGUA FURSA MPYA ZA UTALII NAMTUMBO



Katika bonde la kijani lililojaa mandhari ya kuvutia kusini mwa Tanzania, wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma sasa inang'aa kama nyota mpya ya utalii.

Kupitia uwekezaji wa Shilingi bilioni 2.1 kutoka Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lango la kisasa kuingia Hifadhi ya Taifa ya Nyerere limejengwa eneo la Likuyuseka Maganga na sasa, ndio mlango rasmi wa watalii kuingia hifadhi hiyo kupitia Nyanda za Juu Kusini.

Akizungumza kwa furaha, Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Mheshimiwa Ngollo Malenya, anasema ujenzi wa lango hilo umekamilika na sasa wilaya yake ipo tayari kuwakaribisha wageni kutoka kila pembe ya ukanda wa kusini,ikiwemo mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe, Iringa, Mbeya hadi Ruvuma, na hata nchi jirani kama Msumbiji na Malawi.

"Lango hili ni fursa ya kipekee kwa Namtumbo na Mkoa wa Ruvuma. Linakuza uchumi wetu kwa haraka na linafungua njia ya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya utalii," anasisitiza Malenya huku akitoa rai kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye ujenzi wa hoteli, huduma za utalii na miundombinu mingine muhimu.

### Mlango Mpya, Fursa Mpya

Lango la Namtumbo ni mojawapo ya njia muhimu za kuingia Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, mojawapo ya hifadhi kubwa zaidi Afrika inayochukua zaidi ya kilomita za

mraba 30,000. Hifadhi hii ilianzishwa rasmi mwaka 2019, ikiwa sehemu ya urithi wa zamani wa Selous Game Reserve.

Kupitia lango hili, wageni kutoka mikoa ya kusini sasa wanaweza kufurahia urahisi wa kuingia hifadhi hiyo bila kupitia njia za mbali.

Wageni kutoka Songea, Tunduru na maeneo ya mpakani mwa Msumbiji wanaweza sasa kuingia moja kwa moja kwenye mbuga hiyo tajiri kwa wanyamapori na mandhari ya kuvutia.

Eneo hili linajivunia kuwa na wanyamapori wakubwa kama tembo, simba, chui, nyati, na pundamilia wanaoonekana mara kwa mara katika maeneo ya karibu na lango.

Kivutio kingine ni bwawa la Kaunde, linalofahamika kama bwawa la viboko.Ni bwawa la pekee, lililoko juu ya mlima, na lenye sifa ya kushangaza, maji yake hayakauki mwaka mzima, lakini chanzo chake hakijulikani.

Likiwa limezungukwa na milima na msitu mnene wa hifadhi, bwawa hili limebaki kuwa eneo la asili lisiloguswa, kivutio kwa watalii wa ndani na wa kimataifa wanaotafuta uzuri wa Tanzania.

Isitoshe, Namtumbo inaongeza thamani ya utalii kupitia vivutio vya kiutamaduni. Watalii wanaweza kutembelea vijiji vya Wandendeule na Wangoni na kujifunza historia, mila na utamaduni wa watu wa Ruvuma.

## KAHAWA YALETA MAPINDUZI KIJIJI CHA KINGERIKITI



Wakulima wa kahawa katika Kijiji cha Kingerikiti, Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma wameeleza furaha yao kwa Serikali ya Awamu ya Sita, wakieleza kuwa mabadiliko

ya bei ya zao hilo kutoka Sh. 3,000 hadi Sh. 8,500 kwa kilo yameleta mapinduzi makubwa katika maisha yao. Wamesema hatua hiyo imewawezesha kuinua kipato na kuchochea ari ya kuendelea na kilimo hicho chenye tija.

Mmoja wa wakulima hao, Vitus Mapunda, amesema walikuwa wakikumbwa na changamoto ya bei duni ya kahawa sambamba na gharama kubwa za uzalishaji, hali iliyowafanya kuishi maisha magumu licha ya kufanya kazi kwa bidii mashambani. Ameipongeza Serikali kwa mwelekeo thabiti wa maboresho ya sekta ya kilimo hasa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mapunda amesema kuwa upatikanaji wa mbolea za ruzuku umechangia ongezeko kubwa la uzalishaji wa kahawa kutoka tani nne hadi kufikia tani kumi kwa ekari moja. Mafanikio hayo yametokana na usimamizi makini wa Serikali katika kila hatua ya mnyororo wa thamani wa kahawa, kuanzia maandalizi ya mashamba hadi kwenye masoko.

Pamoja na mafanikio hayo, wakulima wametoa wito kwa Serikali kuongeza idadi ya maafisa ugani hadi ngazi ya kijiji ili kuongeza uelewa wa kilimo bora.

## ZIWA NYASA LILIVYOSHEHENI VISIWA VYA AJABU



Katika wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma, ndani ya kina cha Ziwa Nyasa, kunapatikana visiwa vitatu vya Mbambabay, Lundo na Puulu—hazina ya asili isiyojulikana na wengi. Visiwa hivi si tu mandhari ya kuvutia, bali vinabeba historia,

maisha ya asili na maajabu ya kipekee ambayo yanaweza kuifanya Nyasa kuwa kitovu cha utalii wa kipekee kusini mwa Tanzania.

Kisiwa cha Mbambabay kinajivunia mapango ya kuvutia ambayo hutumika kama hifadhi ya wavuvi wakati wa dhoruba kali. Zaidi ya mandhari, kisiwa hiki ni paradiso ya samaki wa mapambo wanaong'aa chini ya maji safi, huku sauti za ndege na hewa safi vikiumba utulivu wa kuvutia kwa wapenzi wa mazingira ya asili.

Kwa upande mwingine, kisiwa cha Lundo kinahifadhi historia ya maumivu na mafundisho. Enzi ya utawala wa Kijerumani, wagonjwa wa ukoma walipelekwa kisiwani humo kwa ajili ya kutengwa. Makaburi ya waliopoteza maisha yao bado yapo, yakisimulia simulizi ya hofu, imani na mapambano ya kijamii dhidi ya magonjwa.

Kisiwa cha Puulu, kilichopo Kata ya Liuli, ni kivutio kwa watazamaji wa ndege na wapenzi wa uoto wa asili. Samaki wa aina mbalimbali huzaliana humo, lakini nyota wa kivutio ni ndege wa ajabu ajulikanaye kama ngwazi, anayevua samaki kwa ustadi wa kipekee unaovutia watafiti na watalii.

## WANANCHI 900 PERAMIHO WAPATA HUDUMA YA SARATANI



Zaidi ya wananchi 900 wamepatiwa huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani bila malipo katika Hospitali ya Mtakatifu Joseph Peramiho, mkoani Ruvuma, kupitia kambi maalum ya siku nne iliyohusisha madaktari bingwa kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road.


Akizungumza wakati wa ziara yake hospitalini hapo, Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amesema kambi hiyo inalenga kutoa huduma za uchunguzi wa saratani ya matiti, tezi dume na aina nyingine, ikiwa ni sehemu ya juhudi za serikali kupambana na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza.

"Takwimu zinaonesha watu 18 wamekutwa na viashiria vya saratani; kati yao wanawake 12 tayari wameanza matibabu na wanaume sita wamepewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi zaidi," amesema Waziri Mhagama na kumshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha huduma hizo muhimu kwa wananchi.

Ameongeza kuwa utafiti wa Tume ya Saratani (Oncology Commission Report) unaonesha kuwa ifikapo mwaka 2030, idadi ya vifo vitokanavyo na saratani katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara inaweza kuongezeka hadi kufikia watu milioni moja iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Akitaja aina za saratani zinazoongoza hapa nchini, Mhagama amesema kuanzia mwaka 2019 hadi 2024, saratani ya mlango wa kizazi inaongoza kwa asilimia 41, ikifuatiwa na saratani ya matiti kwa asilimia 19, utumbo mkubwa na mdogo asilimia 6.1, koo asilimia 5.7 na saratani ya kichwa na shingo kwa asilimia 4.3.

## LITEMBO IMEJAA HISTORIA YA USHUJAA ILIOZIKWA KATIKA MAJI YA DAMU



Kijiji cha Litembo kilichopo wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, kimeibuka kama kitovu cha historia ya ukombozi barani Afrika baada ya kupatikana kwa kumbukumbu ya mashujaa 800 wa kabila la Wamatengo waliouawa kikatili na wakoloni wa Kijerumani mwaka 1902. Katika kijiji hiki, jiwe kubwa la asili linalofanana na kichwa cha tembo—linalojulikana kama LitembI limegeuka kuwa nembo ya mapambano ya haki dhidi ya bunduki 19 za mkoloni.

Mashujaa hao walipigana kwa mikuki, mishale na mapanga wakijificha nyuma ya jiwe la Litembo, baada ya kukataa kutawaliwa na mjerumani aliyejulikana kama Korongo. Mapambano hayo ya kijasiri yaliambatana na mauaji ya kikatili ambapo damu ya mashujaa ilielezwa kumwagika hadi kuingia mto Mapipa na kuelea hadi ziwa Nyasa, ishara ya mapambano yaliyogharimu maisha ya wengi kwa ajili ya uhuru.

Ndani ya jiwe la Litembo kuna pango la kihistoria linalodaiwa kupita hadi Kijiji cha Maguu, ambalo liliwasaidia baadhi ya mashujaa wachache kunusurika. Pango hilo, ambalo wakazi wanasema lina wanyama wakali, maji, na hata madini ya thamani, limekuwa sehemu ya simulizi ya ajabu, likitazamwa kama maficho ya vita na sasa pia ni sehemu ya kivutio cha kihistoria.

Serikali ya Mkoa wa Ruvuma imejenga mnara wa kumbukumbu karibu na jiwe hilo, ambapo kila mwaka tarehe 28 Novemba huadhimishwa rasmi kuwaheshimu mashujaa hao. Kila kaburi katika eneo hilo linadaiwa kuhifadhi miili ya zaidi ya watu 25, na eneo hilo limekuwa mahali pa ibada ya kihistoria na utambuzi wa mchango wa Wamatengo katika harakati za ukombozi wa nchi.



**RAIS SAMIA AWAPA FURAHA WATOTO WANAOISHI MAZINGIRA MAGUMU RUVUMA**



Mkuu wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Mhe. Simon Chacha, amekabidhi zawadi za sikukuu ya Pasaka kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu mkoani Ruvuma kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, akisema kuwa kitendo hicho ni uthibitisho wa moyo wa upendo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza wakati wa hafla ya ugawaji zawadi hizo zilizotolewa na Rais Samia, Mhe. Chacha amesema hatua hiyo imelenga kuwapa watoto hao furaha na kusherehekea Pasaka kama Watanzania wengine.

Zawadi hizo, zenye thamani ya shilingi milioni 2.688,000, zimegawiwa kwa watoto 182 kutoka wilaya zote tano za Mkoa wa Ruvuma, ambapo kila wilaya ilipokea mbuzi mmoja, mchele kilo 50, sukari kilo 25, maharage, juisi na sabuni za usafi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum na wanaoishi kwenye mazingira hatarishi.

Kwa upande wake, Afisa Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Victory Nyenza, amesema utoaji wa zawadi hizo ni mwendelezo wa jitihada za serikali katika kuunga mkono makundi yenye uhitaji mkubwa, hasa katika nyakati za sikukuu, ili kuwapa faraja na matumaini mapya ya maisha.

## SIMBA ADIMU WA RANGI YA KAHAWIA NA NYEUPE AUAWA MITOMONI



Katika kijiji kidogo cha Mitomoni, kata ya Mipotopoto, pembezoni mwa Pori la Akiba la Liparamba wilayani Nyasa mkoani Ruvuma, tukio la kusikitisha lilitokea wakati simba adimu mwenye rangi ya kahawia na nyeupe alipoingia kwenye makazi ya watu na kusababisha taharuki kubwa. Simba huyu, ambaye ni nadra sana kupatikana duniani, aliuawa baada ya kuvamia nyumba na kufanya uharibifu mkubwa.

Kwa muda mrefu, wakazi wa kijiji hicho walikuwa wakielewa kuwa hifadhi ya Liparamba ni jirani yao, lakini si hatari kwao. Hata hivyo, hali hiyo ilibadilika ghafla siku nne zilizopita.

Diwani wa Kata ya Mipotopoto, Mheshimiwa Said Mahamud, anasimulia tukio la mwananchi mmoja aliyenusurika kifo baada ya kukutana uso kwa uso na simba huyo porini. "Alikuwa njiani kutoka shambani, alipokutana na simba huyo. Aliweza kujiokoa kwa kupanda mti na kutumia matawi kujilinda, kabla ya simba huyo kuondoka," alisema Mahamud.

Hata hivyo, tukio hilo halikuishia hapo. Usiku wa kuamkia Aprili 15, simba huyo alifanya shambulizi la kipekee alipanda paa la nyumba, akashika mbwa, kubomoa dirisha, na kuchukua nguo kabla ya kutoweka gizani. Usiku uliofuata, simba huyo

akaingia zizini na kuua kondoo watano na mbuzi mmoja wa mwananchi Said Njete.

Kwa haraka, Serikali ilichukua hatua kupitia askari wa wanyamapori kutoka Pori la Akiba Liparamba waliowasili kutoka Mbinga. Baada ya ufuatiliaji, waliweza kumuua simba huyo na kuchukua ngozi yake. Mheshimiwa Mahamud alieleza kuwa simba huyo alikuwa dume mwenye rangi ya kahawia na nyeupe, tabia inayowiana na simba adimu wanaopatikana katika Pori la Akiba la Liparamba.

Inasemekana kwamba simba huyu alikuwa dhaifu na mwenye dalili za ugonjwa, jambo ambalo huenda lilimfanya kuvuka mipaka ya pori na kuingia kwenye makazi ya binadamu.

Pori la Liparamba, ambalo linapakana na nchi ya Msumbiji, ni mojawapo ya hazina za kipekee za taifa, likiwa na mandhari ya kuvutia na wanyama adimu kama tembo na simba weupe wa ajabu. Pori hili linatajwa kuwa na uwezo wa kugeuka kuwa moja ya vivutio vikuu vya utalii wa kipekee barani Afrika.

## BILIONI NNE KUNUFAISHA WAKAZI 60,000 MBINGA



Wakazi zaidi ya 60,868 wa kata nane katika Halmashauri ya Mji Mbinga, mkoani Ruvuma, wanatarajia kuondokana na changamoto ya ukosefu wa maji safi na

salama baada ya Serikali kutenga zaidi ya Shilingi bilioni 4.01 kwa ajili ya kuboresha huduma hiyo muhimu.

Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 755.2 zitatumika kumlipa Mkandarasi Kampuni ya Ngogo Engineering Ltd itakayojenga mradi huo, huku zaidi ya Shilingi bilioni 3.25 zikienda kwa Kampuni ya Simba Pipe Industries Ltd kwa ajili ya kutengeneza na kusafirisha mabomba ya maji kutoka kiwandani hadi Wilaya ya Mbinga.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi huo, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbinga Mjini (MBIUWASA), Mhandisi Yonas Ndomba, alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa vyanzo viwili vya maji vyenye uwezo wa kuzalisha lita 1,613,200 kwa siku, matenki manne yenye ujazo wa lita 525,000 na mtandao wa bomba wa kilometa 57.

Amesema Mradi huu utakapokamilika, huduma ya maji katika kata za Ruhuwiko, Mbinga A, Betherehem, Matarawe, Lusonga, Masumuni, Mbinga Mjini B na Mbambi itapatikana kwa asilimia 97.8.

Hata hivyo amesema hivi sasa, mahitaji ya maji katika Mji wa Mbinga ni lita 5,478,000 kwa siku, wakati uzalishaji halisi ni wastani wa lita 3,797,000, sawa na asilimia 69 ya mahitaji, hivyo kuleta upungufu wa lita 1,681,000.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mbinga,Mheshimiwa Kisare Makori, alisisitiza umuhimu wa utekelezaji wa mradi huo kufanyika kwa viwango vya juu na kwa wakati. Alizitaka kampuni husika kutoa ajira za muda kwa wananchi wanaoishi karibu na eneo la mradi, ili kuwawezesha kushiriki moja kwa moja kwenye uboreshaji wa huduma hiyo.



## UJENZI DARAJA MTO RUVUMA WAANZA



Wananchi wa vijiji vya Mkenda na Nakawale katika Halmashauri ya Songea Vijijini pamoja na wananchi wa kijiji cha Mitomoni, Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma, wameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa kuanzisha mradi mkubwa wa ujenzi wa daraja la Mto Ruvuma lenye urefu wa mita 45 na barabara unganishi zenye urefu wa kilomita 8.8.

Msimamizi MKuu wa mradi huo kutoka TANROADS, Mhandisi Fedinandi Mdoe, amesema ujenzi wa daraja hilo tayari umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba 3 mwaka huu, ambapo gharama ya mradi ni Shilingi bilioni 9.293.

Alibainisha kuwa utekelezaji wa mradi huo ulianza rasmi Novemba 7 mwaka jana.

Kwa upande wake, Mhandisi Blanka Mkundelinda, mkaguzi wa vifaa vya ujenzi katika mradi huo, amesema kuwa vifaa vingi vya ujenzi tayari vimepatikana, ambapo baadhi vimepelekwa kwenye maabara za Songea na Dar es Salaam kwa ajili ya vipimo, na vingine tayari vimefikishwa eneo la mradi lililoanza kujengwa.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Salehe Juma, amesema mradi huo unatekelezwa na kampuni ya kizalendo ya Ovans kutoka Wilaya ya Mbinga, na kazi inaendelea vizuri.

Mradi huo umefadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mfuko wa dharura, na wafadhili hao wanataka mradi ukamilike kwa wakati bila kuchelewa, kwani fedha zote za utekelezaji tayari zimeshatolewa

## UZINDUZI WA SHERIA NA KANUNI ZA URUTUBISHAJI CHAKULA




Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe, amezindua rasmi sheria na kanuni za urutubishaji wa chakula za mwaka 2024 katika ukumbi wa Chandamali, Manispaa ya Songea,.

Hii ni hatua muhimu katika kuimarisha afya ya Watanzania kwa kupambana na magonjwa yanayotokana na upungufu wa virutubisho.

Katika uzinduzi huo, Mhe. Kigahe alisisitiza kuwa sheria na kanuni hizo zinalenga kuhakikisha chakula kinakuwa na virutubisho muhimu kama njia ya kudhibiti matatizo ya lishe, hasa utapiamlo, udumavu, na upungufu wa vitamini.

“Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alisaini mkataba wa lishe mwaka 2022 na kutoa maelekezo kwa Wizara yetu kuandaa kanuni hizi ili kukabiliana na changamoto za lishe duni,” amesema Kigahe.

Vyakula vinavyolengwa katika mpango huu wa urutubishaji ni pamoja na unga wa mahindi, unga wa ngano, mafuta na chumvi, ambavyo vitatakiwa kuongezewa virutubisho muhimu kwa afya ya binadamu.

Mhe. Kigahe aliwasihi wadau kutoka sekta mbalimbali kushirikiana katika utekelezaji wa sheria hizi na kuwataka wazalishaji kujiandaa mapema kwa mabadiliko hayo.

## ALICHOKISEMA BALOZI NCHIMBI KWA WANAHABARI SONGEA




Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, ametoa wito kwa wahariri na waandishi wa habari kuandika habari zinazojenga mshikamano katika taifa na sio zinazochochea chuki.

Ametoa wito huo wakati akifungua mkutano maalum wa jukwaa la wahariri Tanzania (TEF) uliofanyika katika ukumbi wa Kanisa Katoliki la Bombambili, uliopo manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

"Wahariri wa vyombo vya habari ambao ndio mnaruhusu habari yoyote itoke kwenye chombo cha habari, kama mngetumia nafasi zenu vibaya inawezekana nchi isingekuwa kama ilivyo leo, wahariri ndio chujio la habari zote katika taifa, kwa siku zote ambazo mmetimiza wajibu wenu mmefanya taifa letu kuwa na utangamano," alisema Dkt. Nchimbi.

Dkt. Nchimbi ameeleza kuwa vyombo vya habari vinatakiwa kuhakikisha vinakemea wanasiasa wa upande wowote anayetamka mambo ambayo yanaweza kusababisha vurugu au maumivu kwa raia na hata kupelekea vifo.

Pamoja na mambo mengine katika mkutano huo, amepongeza juhudi za Jukwaa la Wahariri kwa kuendesha uchaguzi wa viongozi wake kwa misingi ya demokrasia na uwajibikaji, akisema kuwa ni mfano mzuri wa taasisi zinazoendeshwa kwa uwazi na ushirikishwaji.

Naye Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mhe. Hamis Mwinjuma, amesema wizara itaendelea kusimamia uhuru wa vyombo vya habari

na maslahi ya wanahabari na wataendelea kushirikiana na wadau wa sekta hiyo ili kuhakikisha mazingiza bora ya uendeshaji wa vyombo vya habari nchini.

## DKT.NCHIMBI ALIVYOZINDUA JARIDA LA MKOA WA RUVUMA




Pichani Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, akizindua jarida maalum la mkoa wa Ruvuma linaloonyesha mafanikio ya miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika sekta mbalimbali mkoani Ruvuma.

Uzinduzi huo umefanyika leo, Aprili 4, 2025, katika Mkutano Mkuu Maalum wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), uliofanyika kwenye Ukumbi wa Kanisa Katoliki Bombambili, Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma,

Jarida hilo linatoa taswira ya maendeleo makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia, katika sekta mbalimbali ikiwemo afya, elimu, maji pamoja na barabara.

## WANAHABARI WAJENGEWA UWEZO SONGEA



Wizara ya Afya imeendesha semina kwa waandishi wa habari na wadau wa lishe mkoani Ruvuma ambayo imelenga kuwaongezea ujuzi ili waweze kufikisha ujumbe sahihi na kuielimisha jamii juu ya matumizi ya chakula kilichoongezwa virutubishi.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dr. Louis Chomboko, akifungua semina hiyo kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa, amesema baada ya semina hiyo waandishi wa habari na wadau wa lishe wanatarajiwa kuwa wahamasishaji wa kanuni za uongezaji virutubishi kwenye vyakula ili kupunguza tatizo la upungufu wa madini na vitamini katika mkoa wa Ruvuma.

Amebainisha kuwa kwa mujibu wa takwimu za afya na viashiria vya malaria za mwaka 2022, hali ya udumavu katika mkoa wa Ruvuma ni asilimia 35.6, uzito pungufu ni asilimia 12.2, upungufu wa damu kwa watoto walio chini ya miaka 5 asilimia 45 na upungufu wa damu kwa wajawazito asilimia 30.



JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA
Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

S.L.P 74 SONGEA
57180 RUVUMA
SIMU Nambari. 025-2602256/2602238
FAX Na. 2602144
E -MAIL:ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
TOVUTI: www.ruvuma.go.tz
INSTAGRAM: rs ruvuma
FACEBOOK: rs ruvuma
YOUTUBE: rs ruvuma